

# HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

Barua Zote Zitumwe Kwa Mkurugenzi Wa Halmashauri

S.L.P 30112  
SIMU Na: 023 - 240 2886  
FAX Na: 023 - 240 2007  
td@kibahatc.go.tz



OFISI YA MKURUGENZI  
WA MJI KIBAHA

28/05/2018

## TANGAZO LA MNADA WA MAGARI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha anawatangazia Wananchi wote kuwa kutakuwa na mnada wa hadhara wa kuuza magari chakavu ya Halmashauri ya Mji Kibaha utakaofanyika eneo la **Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani** na **Ofisi ya Polisi (W) Kibaha** siku ya **Alhamisi tarehe 14/06/2018** kuanzia **saa 5:00 asubuhi**. Orodha ya mali hizo zimeainishwa katika jedwali hapa chini:

S/N	LOT NO	NAMBA YA USAJILI	AINA YA GARI	ENGINE NO	HALI YA GARI	ENEO LILIPO GARI
1	CR/KTC/MV/2017/18/1	SM 3265	SPORTAGE	FE - 114989	HALITUMIKI	Polisi (W) Kibaha
2	CR/KTC/MV/2017/18/2	SM 3759	TOYOTA HILUX D/CABIN	3L- 5251255	HALITUMIKI	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Pwani
3	CR/KTC/MV/2017/18/3	SM 2939	TOYOTA L/C HARDTOP	IHZ - 0323009	HALITUMIKI	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Pwani
4	CR/KTC/MV/2017/18/4	SM 3231	ISUZ FSR	297395	HALITUMIKI	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Pwani
5	CR/KTC/MV/2017/18/5	SM 4179	NISSAN PATROL S/W	TD42 - 177165	HALITUMIKI	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Pwani
6		SM 4976	NISSAN HB/PICKUP	ZD30106917K	HALITUMIKI	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Pwani

### MASHARTI YA MNADA

1. Mnunuzi atakayefika bei ya juu kuliko wote ndiye atakayekuwa mnunuzi halali katika mnada huo na atatakiwa kulipa 25% ya bei aliyofikia baada ya nyundo ya dalali kuangushwa, na atamalizia salio la 75% ndani ya siku 14 baada ya mnada. Mnunuzi atakayeshindwa kulipa 75% ndani siku 14, ushindi wake utafutwa na hatarudishiwa kiasi alichotanguliza, na mali hiyo itauzwa tena.
2. Ukaguzi wa magari utafanyika siku mbili kabla ya siku ya mnada kuanzia **saa 5: 00 asubuhi hadi saa 8: 00 mchana** katika **Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Pwani**.
3. Magari yatauzwa jinsi yalivyo ,yanavyoonekana, na mahali yalipo.
4. Mnunuzi atakayenunua chombo cha moto atawajibika kulipia kodi zitakazotakiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.
5. Mnada utafanyika siku ya **Alhamisi tarehe 14/06/2018** kuanzia **saa 5:00 asubuhi**
6. Gharama zote za kuhamisha na kusafirisha gari au kifaa chochoe zitakuwa kwa mnunuzi.

Jenifa C. Omolo  
Mkurugenzi  
Halmashauri ya mji Kibaha

Kwa mawasiliano zaidi fika ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Mji Kibaha, Ama wasiliana kwa S.L.P 30112 Kibaha, Pwani au tembelea tovuti ya [www.kibahatc.go.tz](http://www.kibahatc.go.tz)